

## JINSI YA KUWASILISHA MAOMBA

Miradi ya udugu inayokidhi sifa zilizotajwa hapo juu inaweza kutuma maombi ya tuzo ya udugu kwa mwaka 2021. Kipaumbele katika kuchagua miradi bora kitatolewa kwa ile yenye matumizi ya kibunifu (kwa mfano video, mahojiano n.k.) Mwisho wa kutuma maombi ya miradi kwa UEM ni tarehe **15 Machi 2021** kwa barua pepe: [Partnerships@vemission.org](mailto:Partnerships@vemission.org)

## MAWASILIANO:

### Zakaria Mnkai

United Evangelical Mission  
Regional Office Africa  
Sokoine Drive  
Luther House, Second floor  
PO Box 75240 Dar es Salaam  
Tanzania  
✉ [Mnkai-Z@vemission.org](mailto:Mnkai-Z@vemission.org)

### Petrus Sugito

United Evangelical Mission  
Regional Office Asia  
Jl. Pdt. J. Wismar Saragih  
Bane, Kec. Siantar Utara  
Kota Pematangsiantar  
North Sumatra 21142  
Indonesia  
✉ [Sugito-P@vemission.org](mailto:Sugito-P@vemission.org)

### Frauke Bürgers and Kristina Neubauer

United Evangelical Mission  
Rudolfstrasse 137  
D-42285 Wuppertal  
Germany  
✉ [partnerships@vemission.org](mailto:partnerships@vemission.org)



Mwanachama wa  
**actalliance**



## TUZO YA UDUGU 2021

United Evangelical Mission  
Rudolfstrasse 137  
D-42285 Wuppertal  
☎ +49 (0) 202 890 04-0  
☎ +49 (0) 202 890 04-179  
✉ [partnerships@vemission.org](mailto:partnerships@vemission.org)  
[www.vemission.org](http://www.vemission.org)

Facebook [@VEMission](https://www.facebook.com/@VEMission)

Instagram [@unitedinmission](https://www.instagram.com/@unitedinmission)

YouTube [United Evangelical Mission](https://www.youtube.com/UnitedEvangelicalMission)

### Waliohusika

Mchapishaji: United Evangelical Mission (UEM)  
Mhariri: Brunhild von Local  
Michoro: Britta Kläffgen  
Layout: MediaCompany GmbH  
Toleo hili: Februari, 2020





## MAELEZO JUU YA TUZO


Chama cha Misioni cha UEM kitatua mradi bora wa kidugu Afrika, Asia na Ujerumani kwa mwaka 2021. Tuzo ya udugu, 2021 itazingatia miradi iletayo furaha na kuzingatia “hisia zote tano” zilizopendekezwa na Mkutano wa Udugu wa Kimataifa wa mwaka 2017. Miradi bora yenye mada “Furaha katika udugu” itakayoshinda tuzo itawasilishwa katika Mkutano Mkuu wa 2021 na kutuzwa kiasi cha pesa kati ya euro mia tano hadi elfu mbili.

## SIFA ZA WAOMBAJI

Vikundi vyote vya udugu vya UEM vinakaribishwa kuwania tuzo hii.

## BARAZA LA WATOA TUZO

Kamati ya udugu ya UEM itaamua miradi itakayopokea tuzo ya udugu.



## VIGEZO

1. Mradi unasisitiza “Furaha katika Udugu” kuwa lengo muhimu (tazama mapendekezo kutoka Mkutano wa Kimataifa wa Tatu wa UEM wa mwaka 2017).
2. Mradi unajumuisha “hisia zote tano”.
3. Mradi wa kibunifu (kwa mfano: udugu unaoundwa na pande tatu).
4. Kundi lengwa limehusishwa tangu mwanzo wa mradi.
5. Mradi unazingatia **vigezo** vya miradi ya UEM, yaani:

### Uamuzi wa pande husika

Ni sharti kuwa uamuzi wa kushiriki katika maombi ya tuzo ya udugu ya UEM yafanyike na pande zote za udugu.

### Mipango, ufuatiliaji na tathmini jumuishi

Mradi umetekelezwa kwa kuzingatia upangaji, ufuatiliaji na tathmini jumuishi (PME).

### Uandaaji wa mradi kuzingatia misingi mbalimbali

Katika kupanga mradi, angalau misingi miwili ya kazi ya UEM kati ya hii mitano izingatiwe:

Msaada wa kisheria/ Utetezi  
Diakonia  
Maendeleo  
Uinjilisti  
Udugu

Pale inapowezekana, mradi uandaliwe kwa dhuni la kujumuisha pande zote za udugu.

### Utekelezaji wa kielimu

Makanisa, vikundi na taasisi katika nchi shiriki ziunge mkono mradi kwa kutoa semina, mikutano, matukio na shughuli nyingine kwa watu wao.

### Taarifa kwa umma

Makanisa na/au vyombo vya habari visivyo vya kikanisa vitaripoti kuhusu matukio, semina na shughuli nyingine za mradi wakati unatekelezwa.

## TUZO ZA PESA

Mshindi wa kwanza atatuzwa euro elfu mbili, mshindi wa pili atatuzwa euro elfu moja na mshindi wa tatu atatuzwa euro mia tano.